

(R 1922)

## INJILI YA YESU MLIMANI

Luka 6:41-49

NAKALA MUHIMU\_ 'Kwa nini mnaniita Bwana Bwana nanyi hamfanyi ninavyowaambia ?' \_Luka 6:46

Haya maneno ya Yesu mlimani yanatufunulia mambo kadhaa muhimu :-(1)Sio vema kuhimiza ndani yako tabia ya kumtautia mwenzio makosa ambalo kwako wewe waona ni kosa bali kwake sio kosa ,ikiwa sio la kwetu ,lazima yafichuliwe na mara nyingi yanatumiza .

Upendo wa kweli kwa undungu ni lazima tufahamu kuwa kila mtu ana dosari, wakati mwingine makosa ya majirani yetu hayatufurahishi pia yetu yanaweza kuwa hayawafurahishi wao pia;na tunapotamani kuwa na majirani zetu wakijali kilema chetu kutoka anguko na kuwa na uvumilivu na udhaifu wetu,kwa hivyo katika upendo huo huo wa kindugu ,tunapaswa pia nasi tuwe na uvumilivu kama huo.

(2)Maneno ya Bwana yanamaanisha kwamba tabia ya kuendeleza kuhesabia wengine kosa na sisi wenyewe hatujajichunguza kwanza, tutakuwa wanafiki-tutakuwa wenyе bidii ya haki ambayo sio ya ukweli.Bidii ya dhati kwa haki daima itaanza na nidhamu ya kibinagsi;na kwa kuendelea kusaidia wengine,watajitatihidi kufanya hivyo kwa ustadi na uangalifu na kwa upole iwezekanavyo,kukumbuka michakato ya polepole na urchungu wa kujirekebisha mwenyewe na utamaduni wa kibinagsi.

Ikiwa mtu ye yeyote hatapeana moyo wake mwenyewe kwa uongozi na mafundisho ya Mungu, hatakuwa na mamlaka kutoka kwake ya kuwafundisha wengine kufanya hivyo.Na kwa wale ambao wanadhania kufanya hivyo kama mafarisayo na walimu wa sheria ni unafiki,kama Bwana alivyoonyesha wazi(Mat 23 : 2\_7,13)"Kwa waovu wale ambao mnaojua ukweli na hamyatendi kulingana na mafundisho mnayoyafundisha )Lakini kwake mtu mwovu Mungu asema una haki gani kunena sheria zangu na kuchukua agano mdomoni mwako?una chukia mafundisho yangu na kuyatupa maneno yangu nyuma yako .(Zab 50: 16,17).Wale tu ambao wamewekwa wakfu kamili kwa bwana wamepokea upako wa Roho wake Mtakatifu.Wameagizwa na Mungu kuhubiri injili na kuhudumu katika nyumba ya imani.Na ni wale tu wanaoendelea kujinyenyekeza kwa uaminifu kwa uongozo wa Roho Mtakatifu;kutoka kwa njia za zamani za dhambi na uchafu na kuelekea katika njia za utakatifu,yanayostahili au yanayoweza kufanya huduma ya ustadi na kufundisha na kutumikia katika nyumba ya bwana.

(3) Neno latueleza kwamba katika maisha yetu lazima tuchunge /tuwe makini katika maneno na matendo ya kawaida ya kila siku kama faharisi ya miyo yetu . Akisema, "Hakuna mti mzuri uwezao kuzaa matunda mabaya au mti mbaya kutoa matunda mazuri ,kwa kuwa mti hujulikana pindi tu itakapozaa matunda yake." Vivyo hivyo mtu mwema hutoa mambo mema kutoka kwenye hazina ya moyo wake,naye mtu mwovu hutoa mambo maovu kutoka kwenye hazina ya moyo wake,kwa kuwa mtu hunena kwa kinywa chake yale yaliyoujaza moyo wake."

Kwa hivyo inaoneka kwamba maneno au matendo yetu yote kwa uchache ama katika mambo makuu ya maisha yanashuhudia katika hukumu,iwe kwa sisi au dhidi yetu kwa maisha yetu ya kila siku tuwe waangalifu kwa kujilinda kwa kila tendo na neno la uzima :na ikiwa tutapatikana kwa kosa lolote,tunapaswa kutubu haraka na kutafuta msamaha ,tukikumbuka kwamba "mtu ye yote akifanya dhambi ,tuna wakili wetu."na kadhalika.1 Yohana 2:1'2

(4) Tumeitwa basi kuwa wenyewe kusikia na kutenda neno la Mungu, kufanya jinsi Bwana ametuonyesha,kumaanisha sio onyesho la kweli ya haki (kutilia maanani matendo mema ya mtu kwa kulinganisha na anguko kwa wengine na wakati mtu anapokuwa kipofu asiweze kuona hata makosa ya kina na makosa ambayo yanamhusu,lakini inamaanisha mageuzi makubwa ya kina .Kujichunguza kwa undani kabisa ili tuweze kuondoa uchafu wote wa kiburi na majivuno na kuweka msingi vizuri ya tabia ya kweli na haki.Kuweka msingi imara juu ya kuunda muundo kama huo,hatuwezi weka msingi imara hadi tutakapomjia yesu kristo mwamba.(1 Kor 10: 4,Rum 9:33,1 Pet 2:7\_8)Kwa uwezo wetu wenyewe hatuwezi kupata msingi wetu imara ambao tunaweza kujenga tabia na imani yetu .Wala hakuna kuimarika katika jambo lolote ambalo watu wengine wanaweza kutengeza .

Maazimio ya wanadamu na nadharia za wanadamu yote ni msingi ya mchanga ambayo hayawezi kudumu katika dhoruba za maisha.Lakini wale walio na mzizi na msingi katika Kristo na kujengwa ndani yake -katika mafundisho yake ,upendo wake na tabia yake-hawawezi kutingizwa kamwe.Mafuriko ya majoribu yanapoinuka na katika kijito thabiti kikipiga dhidi ya nyumba hiyo haitahamishwa ,kwa kuwa nguvu yake iko katika Kristo,mwamba thabiti amabao umejengwa juu yake.

Wale ambao hawajajengwa kwa Kristo hakika wataanguka:imani yao itaondolewa;na tabia yao lazima itakuwa na shida ya kupungua kwa imani yao.